**TANZANIA NETWORK OF WOMEN**

**LIVING WITH HIV AND AIDS**

Tabata Area, Bandari Street, House No.34

web:www.tzpositivewomen@net.


# SARATANI YA VIA VYA UZAZI

# Malengo

Baada ya somo hili mshiriki ataweza;

- Kueleza dhana ya Saratani za via vya **UZAZI**
- Kueleza kwa muhtasari sababu zinazochangia kupata saratani ya mlango wa kizazi, dalili za ugonjwa na jinsi ya kujikinga
- Kueleza sababu zinazochangia kupata saratani ya matiti, dalili za ugonjwa na jinsi ya kupunguza uwezekano wa kupata
- Kuelimisha wateja sababu zinazochangia kupata saratani ya tezi dume, dalili za ugonjwa na jinsi ya kupunguza uwezekano wa kupata saratani hii

# Malengo:

- Kutoa unasihi kwa wateja kuhusu umuhimu wa kufanya uchunguzi mapema kuzuia saratani za via vya uzazi na kuonyesha kwa vitendo namna ya kujichuguza Saratani ya matiti
- Kutambua majukumu na wajibu wa wahudumu wa afya ngazi ya jamii katika kutekeleza mpango wa kitaifa wa kupunguza vifo vitokanavyo an Saratani za via vya uzazi
- Kutambua wateja wanaotakiwa kupewa rufaa kwa ajili ya uchunguzi wa saratani za via vya uzazi
- Kutoa ushauri kwa familia na jamii kwa ujumla kusaidia wagonjwa waliogunduliwa na Saratani za via vya uzazi
- Kuainisha imani na fikra potofu ndani ya jamii kuhusu Saratani za via vya uzazi

# Bunga Bongo/Majadiliano

- Saratani za via vya uzazi;
  - Mnaelewa nini ?
  - Mmeshawahi kumwona mgonjwa wa saratani ?
  - Je alikuwa na dalili zipi ?


# DHANA YA SARATANI ZA VIA VYA UZAZI

- Saratani ni ugonjwa unaosababishwa na ukuwaji wa chembechembe hai za mwili bila mpangilio (uvimbe, kidonda, damu, usaa ,maji maji)
- Saratani za via vya uzazi ni tatizo kubwa la afya kwenye jamii ya watanzania.
- Saratani hizi zinaathiri viungo vya uzazi vya mwanamke au mwanamme
- Saratani hizi zinajumuisha; saratani ya mlango wa kizazi,matiti na tezi dume.
- Wizara ya Afya imeweka mikakati mbali mbali ya kupambana na Saratani hizi.

# SARATANI YA MLANGO WA KIZAZI

- Mlango wa kizazi (*cervix*) ni sehemu ya mfuko wa kizazi kuelekea kwenye njia ya uke.
- Sehemu hii ina kazi nyingi ikiwemo;
  - kupitisha mbegu za kiume kuelekea katika mirija ya uzazi
  - kupitisha damu ya hedhi
  - ndio mlango anapopita mtoto wakati wa kuzaliwa kutoka katika mfuko wa uzazi.
- Saratani ya mlango wa kizazi ni aina ya saratani inayoshambulia chembechembe hai (seli) zilizoko kwenye mlango wa kizazi.

# Viungo vya Uzazi wa Mwanamke



# Ukubwa wa Ugonjwa


- Ugonjwa huu unaweza kuwaathiri wanawake wengi na wa rika zote na hasa wale wanaoishi na VVU.
- Duniani kwa takwimu za mwaka 2012;
  - Inakisiwa takriban wanawake 528,000 waligundulika kuwa na saratani ya mlango wa uzazi
  - Kati yao 266,000 walipoteza maisha (nusu yao)
  - Asilimia 85% ya wanaoathirika na ugonjwa huu wanaishi nchi zinazoendelea husuan kusini mwa bara la Africa
- Tanzania:
  - Saratani hii inaathiri wanawake wengi kuliko saratani zote
  - Takriban asilimia 40 ya wagonjwa wapya wenye saratani wanaopewa huduma kutoka Hospitali ya Saratani
  - Ocean Road

# Mlango wa kizazi

Mlango wa Kizazi ulio salama



Mlango wa kizazi ulioathiriwa na saratani/kansa



# Chanzo na Visababishi

- Saratani ya mlango wa kizazi husababishwa na aina ya kirusi kinachoitwa**"Human Papilloma Virus (HPV)"**.
- Kirusi hiki huambukizwa kwa njia ya kujamiiana na mtu mwenye maambukizi
- HPV hupatikana kwa wanawake na wanaume wengi walio katika rika la ujana ambao wameshaanza tendo la kujamiiana
- Huchukua takriban miaka 15-20 kuanzia maambukizi ya kirusi hiki mpaka kansa kujitokeza kwa wanawake
- Mara nyingi mwili huweza kuwaondoa virusi vya HPV kabla ya kuleta madhara yoyote.

# Tabia Hatarishi

- Ni kwa wanawake wachache tu, ambapo virusi vya HPV hukaa muda mrefu kwenye mlango wa kizazi, na baada ya miaka kadhaa husababisha mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi
- Tabia hatarishi;
    - Kuanza ngono katika umri mdogo chini ya miaka 20
    - Uvutaji wa sigara,tumbaku au ugoro
    - Kuwa na wapenzi wengi au kujamiiana na mtu mwenye wapenzi wengi
    - Magonjwa ya zinaa
    - Historia ya kubeba mimba nyingi –takriban zaidi ya tano
    - HIV au magonjwa yanayopunguza kinga za mwili
    - Kutotahiriwa_ **wanaume**

# Dalili za Saratani ya mlango wa Kizazi

- Mabadiliko ya awali (hatua za mwanzo)
  - Hakuna dalili yoyote
  - Mwanamke anaweza kua anaishi bila kujitambua mpaka akifanyiwa uchunguzi ndio tatizo linaweza kuonekana

- Hatua ya saratani;
  - Kutokwa na damu baada ya kujaamiana au wakati wa tendo la ndoa
  - Kutokwa na majimaji au uchafu usio wa kawaida ukeni yenye harufu mbaya
  - Kutokwa na usaha ukeni
  - Kutokwa na damu kidogo kidogo au nyingi ukeni wakati ambao mwanamke hayuko kwenye hedhi
  - Kutokwa na damu ukeni kwa wanawake waliokwisha koma hedhi
  - Maumivu ya tumbo

# Uhusiano: Saratani ya mlango wa kizazi na maambukizi ya VVU

- Mwanamke anaeishi na VVU ana hatari kubwa ya kupata saratani ya mlango wa kizazi kuliko mwanamke asiye na maambukizi.
- VVU huharibu mfumo wa kinga za mwili kujikinga na maradhi na maambukizi ya magonjwa mbalimbali.
- *Kwa wanawake wanoishi na VVU wakipata maambukizi ya HPV, virusi hivi vina nafasi kubwa ya kukaa muda mrefu kwenye mlango wa kizazi na kusababisha saratani.*

# Tunajikingaje kuepuka Saratani ya Mlango wa Kizazi ?

- Kupata chanjo dhidi ya HPV
- Kuepuka ngono katika umri mdogo, chini ya miaka 20
- Kuwa na mwenzi 1 mwaminifu ambaye hana maambukizi ya HPV
- Kutumia kondomu kila unapofanya tendo la kujaamiana
- Kuepuka uvutaji wa sigara,tumbaku au ugoro
- Kuepuka kubeba mimba katika umri mdogo
- Kuepuka kubeba mimba nyingi zaidi ya mara 5
- Wanaume kushiriki kupunguza maambukizi ya HPV kwa kutahiriwa
- Kuchunguzwa saratani ya mlango wa kizazi mara kwa mara ili kubaini mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi yaweze kutibiwa

# Utajuaje kama una saratani ya mlango wa kizazi

- Katika mabadiliko ya awali, ugonjwa huu huwa hauna dalili yeyote!

- Ni muhimu kuwahimiza wannanchi kujitokeza kwenda katika vituo vya kutolea huduma kufanya uchunguzi wa mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi

# Nani anayepaswa kufanyiwa uchunguzi ? Vigezo vya kuzingatia

| Mwanamke anayepaswa kupima | Mwanamke asiyepaswa kupimwa |
|---|---|
| Mwenye umri kati ya miaka 30 na 50 | Mama mjamzito<br>***Apime miezi mitatu baada ya kujifungua |
| Mwanamke yoyote anayeishi na maambukizi ya virusi vya UKIMWI bila kujali umri mradi awe ameanza kujamiiana | Mwanamke aliye kwenye siku zake (hedhi)<br>**Apime baada ya hedhi kumalizika |
| Mwanamke yoyote ambaye hajawahi kuchunguzwa saratani ya mlango wa kizazi | |
| Mwanamke ambaye ameshachunguzwa na anahitaji ufuatiliaji | Ambaye ameshachunguzwa kwa sasa hana tatizo na muda wa kurudia uchunguzi bado haujafika kulingana na vigezo |
| Mwanamke mwenye mlango wa kizazi | Mwanamke aliyetolewa mlango wa kizazi |
| Mwenye dalili za saratani : kutoka damu baada ya kujaamina,kutoka damu bila mpangilio,kutoka uchafu na maji maji ukeni | |

TNW+

# SARATANI YA MATITI



- Inawaathiri wanawake wengi Tanzania.
- Wanawake wengi wanapata tatizo hili kuliko wanaume.
- Inakadiriwa kati ya wagonjwa 100 wenye Saratani ya matiti,mmoja atakuwa mwanaume (10%).
- Takwimu za ulimwengu zinaonyesha takriban;
  - Asilimia 14.4% waligunduliwa na Saratani ya matiti mwaka 2012 Tanzania.
  - Kutokana na takwimu za Hospitali ya Ocean road, wanawake wengi wanafika kupata huduma hii wakiwa katika ngazi za juu za ugonjwa

TNW+ TANZANIA NETWORK OF WOMEN LIVING WITH HIV/AIDS

# Saratani hii inasababishwa na nini ?

| Visababishi ambavyo havizuiliki | Visababishi ambavyo unaweza kujikinga |
|---|---|
| • Jinsia-mwanamke | • Kutokunyonyesha watoto kwa muda mrefu (angalau miaka 2) |
| • Umri-umri hatarishi wa kupata saratani ya matiti ni zaidi ya miaka 45 | • Matumizi ya pombe |
| • Historia ya Saratani ya matiti kwenye familia | • Kutokuzaa kwa hiari |
| • Historia ya kutokuzaa; wanawake ambao hawajajaliwa kupata watoto wana uwezekano mkubwa wa kupata saratani hii | • Kuacha kula matunda na mboga mboga |
| • Kupata hedhi kwenye umri chini ya miaka 12 na kuchelewa kufunga hedhi zaidi ya miaka 55 | • Kuepuka kufanya mazoezi |

# Je, dalili za saratani ya Matiti ni zipi?

- Kivimbe katika titi au kwapani kisichokuwa na maumivu
- Mabadiliko katika umbo au ukubwa wa titi
- Mabadiliko ya ngozi ya titi (kuwa kama ganda la chungwa)
- Kutokwa na majimaji machafu au damu katika chuchu
- Mabadiliko katika chuchu kama vile chuchu kuvutwa ndani ya titi
- Kidonda kwenye titi



# Njia za kupunguza kupata Saratani ya Matiti

- Kujichunguza mwenyewe matiti yako mara kwa mara
- Kufanyiwa uchunguzi wa matiti angalau mara moja kwa mwaka kwa wanawake wenye umri kuanzia miaka 40 katika kituo cha kutolea huduma za afya
- Kupunguza/kuacha matumizi ya sigara na tumbaku
- Kupunguza/kuacha matumizi ya mafuta kwa wingi kwenye chakula hasa yale yatokanayo na wanyama na kula mboga mboga kwa wingi
- Kula mbogamboga na matunda mara kwa mara
- Kufanya mazoezi mara kwa mara




# SARATANI YA TEZI DUME




- Tezi dume:
  - Ni kiungo kwenye mfumo wa uzazi wa wanaume chini ya kibofu cha mkojo
  - Huzunguka mrija ambao hutumika kupitishia haja ndogo kutoka kwenye kibofu kwenda nje
  - Ni tezi inayotengeneza majimaji ambayo huchanganyika na shahawa
- Saratani ya tezi dume;
  - Chembe chembe hai za tezi dume zinakua bila mpangilio
  - Ugonjwa huu umekua ukiongezeka kwa miaka kadhaa iliyopita nchini Tanzania.

# TEZI DUME


UKWELI KUHUSU SARATANI YA TEZI DUME
Hivi karibuni, Mhe.Rais J. Kikwete aligundulika kuwa na Saratani ya Tezi Dume, akafanyiwa upasuaji na kupona kabisa, hii ni kwa sababu aliwahi kupata matibabu.
Je, unataka kujua ukweli juu ya saratani hii ili ujiepushe nayo? Madaktari bingwa watakushauri.
Tuma neno
DAKTARI kwenda
15542
Pamoja na mambo mengine
utapata ushauri juu ya Saratani ya Tezi Dume.
Tezi
Dume
★ Kwa wateja wa vodacom pekee.


Kibofu
Puru
Tezi dume

# TEZI DUME




- Ripoti ya mwaka 2012 ilikadiria wagonjwa wapya 3434 waligunduliwa na Saratani hii duniani
  - Ni takriban asilimia 10 ya wagonjwa wote wa saratani.
- Takwimu kutoka Taasisi ya Saratani Ocean Road zinaonyesha;
  - Idadi ya wagonjwa imekua ikiongezeka
    - Mwaka 2006 wagonjwa 51 walitibiwa
    - Mwaka 2013 wagonjwa 116 walifika Hospitali ya Ocean Road kwa ajili ya matibabu

# Nani anaweza kupata saratani ya tezi dume?

- Mwanaume yeyote mwenye umri wa kuanzia miaka 45 na kuendelea
- Mwanaume mwenye baba, kaka au ndugu wa kiume katika familia ambaye alishawahi kupata Saratani ya Tezi Dume

# Dalili za Saratani ya Tezi Dume

- Kutoa haja ndogo mara kwa mara mchana na usiku
- Kupungua kwa haja ndogo
- Kujisikia kutomaliza haja ndogo baada ya kumaliza kukojoa
- Kushindwa kuitoa haja ndogo yote katika kibofu
- Maumivu wakati wa kwenda haja ndogo
- Kutoa damu katika haja ndogo
- Maumivu ya muda mrefu eneo la kiuno, chini ya tumbo au mgongo.
- Maumivu makali yanaweza kujitokeza katika eneo husika kama saratani itasambaa kwenye viungo vingine

# Kupunguza uwezekano wa kupata Saratani ya Tezi Dume

- Jamii inaweza kupunguza uwezekano wa kupata saratani ya tezi dume kwa kuwashauri wanaume;
    - Kufanya uchunguzi na tiba ya Saratani ya tezi dume mara kwa mara
    - Kufika kituo cha kutolea huduma za afya mara waonapo dalili za saratani ya tezi dume

## Majukumu ya wahudumu wa afya ngazi ya jamii katika kutekeleza mpango wa kitaifa wa kupunguza vifo vitokanavyo na Saratani za via vya Uzazi

- Kuhamasisha jamii kufanya uchunguzi wa Saratani za via vya uzazi
- Kuelemisha jamii umri wa kufanyiwa uchunguzi
- Kuelimisha jamii kuhusu dhana za Saratani za via vya uzazi
- Kuhamasisha ushiriki wa wanaume kutoa msaada kwenye jamii
- Kuelimisha jamii kuhusu imani na mila potofu
- Kutoa rufaa kwa wakati unaostahili
- Kuelimisha familia na jamii jinsi ya kuwatunza na kuwajali wagonjwa wanaongunduliwa na Saratani
- Kufanya ufatiliaji na kuwakumbusha wateja na wagonjwa kuhusu upimaji na muda wa mahudhurio

# Rufaa kwa ajili ya Uchunguzi wa Saratani ya via vya Uzazi (Walengwa)

| Mlango wa Kizazi | Matiti | Tezi Dume |
|---|---|---|
| Wanawake wenye umri wa miaka 30-50 kufanya uchunguzi wa awali | Wanawake wenye dalili za Saratani. | Wanaume kuanzia miaka 45 (wale wenye historia ya Saratani hii kwenye familia) na kuanzia miaka 50 kwa wale wasio na historia ya Saratani hii kwenye familia kufanya uchunguzi wa saratani ya tezi dume |
| Wanawake wenye dalili za Saratani | Wanawake wenye umri zaidi ya miaka hamsini na kuendelea, wapewe rufaa na kukumbushwa kwenda kufanya uchunguzi | Wanaume wenye dalili za Saratani za tezi dume wapewe rufaa ya kwenda vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya uchunguzi zaidi |
| Wanawake waliopata tiba za mabadiliko ya awali kurudi kwa ajili ya hudhurio la marudio | | |
| Waliopata majibu hasi kurudi kwa ajili ya hudhurio la marudio | | |

# Kusaidia wagonjwa waliogunduliwa na Saratani za via vya uzazi

- Ushauri/elimu kwenye familia izingatie;
  - Lishe bora kwa mgonjwa
  - Usafi
  - Umuhimu wa kwenda kwenye kituo cha kutolea huduma za afya kama mgonjwa hali yake sio nzuri
  - Kuonyesha upendo kwa mgonjwa
  - Huduma za kiroho na kisaikolojia pale atakapohitaji
  - Kutoa msaada wa kifedha pale zinapohitajika kuboresha huduma za mgonjwa husika
  - Kuacha unyanyapaa
  - Kuwafuatilia kwa karibu wagonjwa husika na kumwelekeza kupata ushauri wa kisheria atakapohitaji

# Igizo Dhima

## Ushauri kwa familia/jamii kusaidia wagonjwa waliogunduliwa na Saratani za via vya uzazi

- Waombe washiriki watano wa kujitolea kufanya igizo dhima
- Mmoja awe mtoa huduma ngazi ya jamii,wa pili awe mgonjwa wa saratani,mmoja awe baba wa familia na mwingine mama wa familia na wa mwisho jirani
- Angalia maelekezo ya igizo ili kuhakikisha wahusika wanajua majukumu yao katika igizo

# Imani na fikra potofu kuhusu Saratani za via vya uzazi

- Bunga Bongo
  - Jadili mila/fikra  potofu zinazosikika na zinazofahamika kutoka kwenye jamii  kuhusu saratani

# Imani na fikra potofu kuhusu Saratani za via vya uzazi

| IMANI POTOFU | UKWELI KUHUSU SARATANI |
| --- | --- |
| Saratani ya tezi dume inasababishwa na kutembea na mke wa mtu | Hakuna uhusiano wowote kati ya saratani ya tezi dume na kutembea na mke wa mtu |
| Matibabu ya mionzi husambaza Saratani mwilini | Matibabu ya mionzi ni aina ya matibabu ya saratani na wala haisambazi Saratani mwilini |
| Saratani inasababishwa na kulogwa au kutupiwa uchawi | Hakuna saratani inayosababishwa na kulogwa au kutupiwa uchawi |
| Ukipata Saratani huwezi kupona lazima utapoteza maisha | Saratani ikigunduliwa mapema na kutibiwa mgonjwa ana nafasi kubwa ya kupona |
| ▪ Kuwa na kivimbe kwenye titi in maana ni Saratani<br>▪ Saratani ya matiti kuweza kuambukiza<br>▪ Wanaume hawawezi kupata Saratani ya matiti<br>▪ Kutolewa titi husababisha kifo | ▪ Vivimbe 9 kati ya 10 sio Saratani ya matiti<br>▪ Huwezi kuambukiza Saratani ya matiti ya mtu mwingine<br>▪ Asilimia 1 % ya wanaume hupata Saratani ya matiti<br>▪ Kutolewa titi katika hatua za mwanzo za ugonjwa hurefusha maisha |

# Ahsanteni kwa usikivu!!!